KANUNI

# Serikali yazinduka uvuvi Ziwa Victoria

**Waziri Mpina aeleza wabunge Tanzania ilivyoponzwa na sheria yake**

Jesse Mikofu, Mwananchi
jmikofu@mwananchi.co.tz

**Mwanza.** Baada ya wavuvi kuteseka huku wakipoteza mali zao kwa muda mrefu, Serikali inaandaa marekebisho ya dharura ya kanuni kuondoa kikomo cha kuzuia uvuaji na uuzaji samaki wenye urefu zaidi ya sentimita 85 ndani ya Ziwa Victoria kama ilivyo sasa.

Akizungunza katika kikao cha Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ilipotembelea na kusikiliza kero za wadau wa uvuvi jijini Mwanza juzi, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Luhaga Mpina alisema amemuagiza katibu mkuu wa wizara hiyo, Dk Rashid Tamatamah kufanya marekebisho hayo ndani ya mwezi mmoja.

Alisema hatua hiyo itaondoa mianya ya magendo maana samaki hao wanapelekwa nchi za Kenya na Uganda.

Kwa mujibu wa sheria ya uvuvi ya mwaka 2003 na kanuni za uvuvi za mwaka 2009, inaruhusu kuvua sangara kuanzia sentimita 50 na kuendelea lakini isizidi sentimita 85 ilhali Kenya na Uganda sheria zao zinaruhusu.

"Nimeshamwagiza katibu mkuu, kufanya marekebisho ya dharura kuhusu sheria na kanuni hizo maana hatuwezi kusubiria wakati zinaumiza Taifa na wavuvi, hivyo kufikia Aprili 15 mwaka huu nataka niyapate marekebisho hayo mezani kwangu," alisema Mpina.

Licha ya wizara hiyo kuwa kwenye hatua za awali za kuifumua sheria hiyo na kanuni zake, muswada wake wa sheria unatarajiwa kufika bungeni kwa mara ya kwanza kwenye mkutano wa Bunge la bajeti Juni. Hata hivyo, Mpina alisema yapo mambo ambayo hayawezi kusubiri lengo likiwa ni kuokoa sekta ya uvuvi.

Naye msemaji wa Umoja wa Wauza Samaki (Tafu) Sijaona James, alisema changamoto hizo zikiwamo za kufanya operesheni bila utaratibu zinaifanya sekta hiyo ishindwe kukua wakati ingeweza kuchangia asilimia 50 ya pato la taifa.

Mjumbe wa kamati hiyo Professa Sospiter Muhongo, alisema licha ya Tanzania kuwa na sehemu kubwa ya Ziwa Victoria lakini kwa viwanda vya kuchakata samaki inazidiwa na Uganda.

> **"Nimeshamuagiza katibu mkuu, kufanya marekebisho ya dharura kuhusu sheria na kanuni hizo maana hatuwezi kusubiria wakati inaumiza Taifa na wavuvi."**
> Mpina

## Kwa Ufupi

### Vijiji 6 vyapewa elimu ya ufugaji



**Meatu.** Vijiji sita vinavyozunguka Pori la Akiba la Maswa na Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya Makao wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, vimenufaika kwa kuwezeshwa elimu ya vyama vya akiba na mikopo na ufugaji.

Hayo yalielezwa na mkuu wa wilaya ya hiyo Dk Joseph Chilongani akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa mbalimbali vya kuwawezesha wananchi kiuchumi vilivyotolewa na kampuni ya Utalii ya Friedkin Conservation Fund(FCF).

Naye ofisa maendeleo wa jamii ya kampuni ya FCF, Alfred Mwakivike, alisema vijiji zaidi ya 20 vinavyopakana na Pori la Akiba, mashamba ya wakulima yamekuwa yakivamiwa wanyamaporo na kupata hasara.
**(Filbert Rweyemamu)**

# Ukaguzi watajwa kupunguza ajali nchini

Imani Makongoro, Mwananchi
imakongoro@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Madereva wa mabasi wametoa ushuhuda namna ajali za mabasi zilivyopungua huku moja ya vyanzo vilivyosaidia wakikitaja kuwa ni ukaguzi na udhibiti wa mabasi mabovu unaofanywa katika stendi ya mabasi Ubungo (UBT).

Katika stendi hiyo, polisi wamekuwa na utaratibu wa kuyazuia mabasi yanayobainika kuwa na hitilafu baada ya ukaguzi hadi yakarabatiwe.

*Mwananchi* lilitembelea stendi hiyo baada ya robo ya kwanza ya mwaka ikiwa ni baada ya hekaheka za sikukuu za mwisho wa mwaka na kuzungumza na baadhi ya madereva na abiria.

Mbali na madereva kutoa ushuhuda namna ajali za mabasi yatokayo kituoni hapo kupungua, walieleza changamoto iliyopo ya biashara kipindi hiki.

Dereva wa basi la kampuni ya Happy Nation liendalo Arusha Hashim Yusuf, alisema kitendo cha mabasi mabovu kudhibitiwa kituoni hapo kumesaidia

**Wakulima walia,**

SALAMU

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Hamad Masauni (kushoto), akiwaongoza wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama walipowasili jana Chuo cha Polisi Kidatu mkoani Morogoro kwa ajili ya ukaguzi na ushauri wa miradi ya Serikali. **Picha na Wizara ya**

wakikabiliwa na changamoto ya mtoto wa jicho ni wenye kuanzia umri wa miaka 50 na kuendelea na kwa upande wa shinikizo la jicho, hata watoto wadogo wamekuwa wakikumbwa na tatizo hilo," alisema.

wakati wa mkutano na waandishi wa habari wakati akitoa tathmini ya huduma za maji, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya maji nchini.

Alisema kuwa, kwa kuanzia wameanza kutekeleza mradi wa uboreshaji wa mfumo wa maji taka wenye urefu wa kilometa

tutahakikisha huduma hiyo inasogea karibu na wananchi," alisema mkurugenzi huyo.

Hata hivyo, katika kutekeleza sera ya maji, alisema Tanga Uwasa imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya maji katika wilaya za Muheza, Pangani, Mkinga na

"Tumefanikiwa kupeleka mradi wa maji safi katika vijiji vya Mashawe, Kimbo Shembekeza na vijiji jirani ambavyo vipo karibu na Mto Zigi ambacho ndicho chanzo cha maji," alisema mkurugenzi huyo.

mabaraza hayo.

"Mabaraza hayo yamekuwa yakitumiwa kushirikiana na baadhi ya watu wenye uwezo kuhujumu haki za wananchi wanyonge kumiliki ardhi yao kwa kujali masilahi yao.



# KANDA YA ZIWA

MRADI

■ MWANZA

## Mamlaka ya maji Misungwi yanyang'anywa miradi ya maji

Na BENJAMIN MASESE

**WIZARA ya Maji na Umwagiliaji imeinyang'anya baadhi ya majukumu na miradi iliyokuwa ikisimamiwa na Mamlaka ya Maji Wilaya ya Misungwi (Miuwasa).**

**Miradi hiyo imekabidhiwa kwa Mwauwasa iweze kuisimamia na kusambaza maji katika vijiji vilivyopo barabara kuu ya Mwanza-Shinyanya kuanzia Usagara hadi Misungwi Mjini.**

**Uamuzi huo umetolewa baada ya wizara kuridhishwa na utendaji kazi wa Mwauwasa kwa vile imekuwa ya mfano katika kuimamia utekelezaji wa miradi**

■ TARIME

## Wezi wa mifugo wadaiwa kumuua kamanda wa sungusungu

Na TIMOTHY ITEMBE

MKAZI wa Kijiji cha Matamankwe Kata ya Susunu wilayani Tarime, Ayoub Athuman (33) ambaye ni Kamanda wa Sungusungu ameuawa na watu wanaodaiwa kuwa wezi wa mifugo kijijini hapo.

Inaelezwa kuwa watu hao walimvamia wakammwagia lita 20 za petroli na kumchoma.

Tukio hilo lilitokea juzi ikiwa ni siku chache baada ya Diwani wa Kata ya Bumera, Deogratius Ndege (CCM), kuitisha mkutano wa kuwatambua wezi wa mifugo ambao wanawasumbua watu kwa kuwaibia ng'ombe na kutorokea wilayani Tarime na nchi jirani ya Kenya.

Habari zinasema tukio hilo linahusishwa na kile kinachotajwa kuwa alikuwa kikwazo kwa wezi hao kwa vile alikuwa anawazuia kupitisha mifugo katika maeneo ya jirani yake. Akisimulia tukio la kuchomwa moto akiwa anauguza majeraha ya kuungua mwili mzima katika hospitali ya Wilaya ya Tarime, Athuman alisema majambazi hao walifika nyumbani kwake saa 5.00 usiku wa kuamkia Machi 10, mwaka huu wakiwa na petroli kwenye dumu la lita 20.

"Walikuwa kama watu saba wakiwa na petroli lita 20 wakaanza kunimwagia mwilini kisha kuwasha njiti ya kiberiti na moto ukaanza kuniunguza mwili mzima, pia wakaondoka na vitu mbalimbali vya ndani ambavyo thamani yake ni Sh milioni 6.5," alisema.

Athumani alieleza kuwa chanzo cha kuchomwa moto na majambazi hao ni baada ya kuwa anawazuia kupita maeneo anayokaa wakiwa na ng'ombe waliowaiba katika maeneo mbalimbali.

Daktari anayesimamia wodi namba tatu na saba alimolazwa Athuman katika hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tarime, Benard Makonyo alikiri kumpokea mgonjwa huyo akiwa na majereha ya kuunguzwa na moto mwili mzima. Alisisitiza kuwa matukio ya namna hiyo yamekuwa mengi na akawataka wana jamii kuacha kujichukulia sheria mkononi.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Tarime/Rorya, Henry Mwaibambe hakuweza kupatikana kuzungumzia tukio hilo.

PICHA: ALLAN NTANA



■ TABORA

## Wakurugenzi

wa serikali za mitaa ili zitunzwe kwa ajili ya manufaa ya taifa na Afrika.

Aliwataka wananchi na viongozi wa serikali za mitaa kulinda alama zote zilizoko katika maeneo yaliyotumiwa na wapigania uhuru ikiwamo majina katika makaburi na majengo ili kutopoteza kumbukumbu za mashujaa.

Katika hatua nyingine, Waziri Mwakyembe aliwataka wataalamu mbalimbali na maofisa utamaduni nchini, kutumia hazina ya wazee walioko katika maeneo yao wanaojua historia ya kweli kuhusu harakati za kudai uhuru nchini na mapambano ya ukombozi barani Afrika, kupata maelezo na kuyaandika kwa ajili ya kuweka kumbukumbu zake.

"Tunajua kila mtu atakufa, hivyo ni vema tukatumia hazina ya wazee wetu waliopo sasa kupata historia ya kudai uhuru na harakati za ukombozi zilizofanyika nchini ili kuweka kumbukumbu zote zikiwamo picha na maneno yao," waziri huyo aliagiza.

Alisisitiza kuwa simulizi ya wazee ni muhimu katika kuhakikisha hakuna mashujaa walioshiriki harakati za kudai uhuru na ukombozi wa Bara la Afrika zitakazoachwa katika kuandika na kuweka taarifa za kazi zao kihistoria.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (katikati) na Meneja wa QNET Kanda ya Kusini mwa Afrika, Biram Fall (kushoto), waki kata utepe kuzindua rasmi maonyesho ya bidhaa za QNET 2019 katika ukumbi wa Mlimani City jijini humo juzi. Kulia ni Mshauri wa Biashara wa QNET Tanzania, Edward Mkony. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Sheria ya Uvuvi kufumuliwa*

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imelazimika kufanya marekebisho ya dharura kwa baadhi ya vipengele vya Sheria ya Uvuvi kutokana na wananchi kushindwa kuvumilia kusubiri kukamilika marekebisho hayo Julai mwaka huu. Akizungumza jijini Mwanza jana, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, aliwaarifu wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu mpango huo wa serikali walipotembelea viwanda na kuzungumza na baadhi ya wadau wa uvuvi Kanda ya Ziwa.

Wadau waliozungumza na wajumbe wa kamati hiyo ni pamoja na wenye viwanda vya kuchakata samaki, mawakala, wafanyabiashara wa samaki na wauzaji mabondo na zana za uvuvi.

Mpina alisema serikali inafanyia marekebisho Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 kwa dharura kwa baadhi ya vipengele na kufikia Aprili 15, marekebisho hayo yatakuwa yamekamilika.

Mpina aliwaambia wajumbe kuwa vipengele viwili ndivyo vitakavyofanyia marekebisho kikiwamo cha utumiaji wa nyavu za milimita nane kwa uvuaji wa dagaa mchele baharini kwa kuwa awali sheria ilikuwa inataka milimita 10, lakini wakawa wanavulia dagaa papa ambao ni wakubwa. Alisema kutokana na changamoto hiyo, watafanya utafiti ndani ya wiki mbili na ikigundulika kweli milimita nane ndiyo inafaa, watawaruhusu wananchi wavue kwa kutumia nyavu zenye ukubwa huo.

Alisema pia yakifanyika marekebisho kipengele cha upande wa sangara kuangalia kama wana uwezo wa kurekebisha kutoka nyavu zenye ukubwa wa inchi sita hadi saba au nane kwa kuwa inaonekana nyavu zenye matundu ya inchi sita zinavua kwa wingi samaki wa sentimita 50, 75 na 85 kwa kiasi kidogo.

"Katibu Dk. Rashid Tamatamah, ameshapatiwa maagizo na ndani ya wiki mbili, kazi hiyo itakuwa imekamilika," Mpina alisema.

"Baada ya kukumbana na changamoto za wavuvi na kuona hawawezi kuvumilia mpaka ifikapo Julai Mosi, muda wa kukamilika marekebisho ya sheria, tumeona tufanye marekebisho ya dharura kwa baadhi ya vipengele ili ifikapo Aprili 15, viwe vimekamilika kwa upande wa nyavu za sangara iwe inchi saba au nane na dagaa mchele milimita nane," Mpina alisema. Akitolea ufafanuzi suala la utumiaji wa nyavu tofauti kati Dar es Salaam na Mwanza, Mpina alisema uvuvi ni sayansi, hivyo uvuvi wa bahari hauwezi kuwa sawa na wa Ziwa Victoria wala Tanganyika.

Alisema sheria ni moja lakini kanuni ni tofauti kutokana na mazingira kuwa tofauti kwa kuwa ukubwa wa sangara huwezi kuulinganisha na ukubwa wa samaki wanaopatikana baharini na pia dagaa wanaopatikana Ziwa Tanganyika huwezi kulinganishwa na wanaopatikana Ziwa Victoria, hivyo hata zana zinazotumika ni tofauti. Mjumbe wa kamati hiyo, Pascal Haonga, alisema serikali inapaswa kuonyesha namna ya kutatua tatizo na kamati kazi yao itaendelea kuisimamia na kuishauri.

Katibu Mtendaji wa Muungano wa Viwanda vya Uchakataji wa Samaki (TIFPA), Onesmo Sulle, aliiomba serikali kuhakikisha kunakuwa na uwiano wa utekelezaji wa Sheria ya Uvuvi katika nchi zote za Afrika Mashariki.

# OSHA wapunguza gharama za uendeshaji

Na John Nditi, Morogoro

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umepunguza gharama za uendeshaji kwa wawekezaji kwa kuondoa tozo na ada katika maeneo matano ikiwemo urasimu katika kutoa huduma, kujenga uchumi wa viwanda na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala huo, Khadija Mwenda alisema hayo juzi mjini hapa kwenye taarifa yake aliyoiwasilisha kwa Katibu Mkuu katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Andrew Massawe.

Massawe alikuwa mgeni rasmi aliyefungua kikao cha nne cha baraza la tatu la wafanyakazi wa Osha kujadili bajeti na mipango mikakati ya kukabiliana na shughuli mbalimbali za ukaguzi kwa maeneo yao ya kazi kwa mwaka 2019/2020.

Alisema wakala umeweka mkakati endelevu wa mafunzo kwa wakaguzi wake na mwishoni mwa mwaka jana umewapeleka wakaguzi 11 Afrika



viwanda na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Alisema kupitia Wizara ya Viwanda waliandaa andiko la dira ya kufikia malengo hayo kitaifa.

Alitaja maeneo matano yaliyoondolewa tozo na ada ni usajili wa eneo la kazi, kufuta faini zilizokuwa zinahusu vifaa vya kuzima moto na ada ya fomu ya usajili sehemu za kazi.

Pia alitaja nyingine zilizoondolewa usajili wa sehemu za kazi kutoka siku 14 hadi siku moja na upatikanaji wa leseni ya kukidhi sheria ya usalama na afya makali pa kazi kutoka siku 28 hadi siku tatu.

Alisema kutokana na mabadiliko hayo kuna ongezeko la sehemu za kazi 8,392 zilizosajiliwa na Osha mwaka 2018 ukilinganishwa na sehemu za kazi 2,845 zilizosajiliwa kwa mwaka 2015.

Alisema mabadiliko yameiongeza leseni za kukidhi usalama na afya mahali pa kazi kutoka leseni 106 kwa robo moja ya mwaka 2017 hadi leseni 210 kwa robo moja ya mwaka 2018.

"Chini ya mpango huu wa kujitathimini wa miaka mitatu tumeweza kuwafikia walengwa wengi na kuongeza makusanyo ya mapato na usalama wa afya ili kuongeza tija," alisema.

Alisema serikali iligharamia mafunzo kwa wenye viwanda vidogo, wajasiriamali wadogo na vikundi vya walemavu kwa usindikaji wa vyakula, ushonaji na utengenezaji batiki 16,897 zaidi ya lengo la wajasiriamali na wenye viwanda vidogo 12,000.

Mafunzo hayo yalifanyika mikoa ya Tabora, Mtwara, Ruvuma, Dodoma, Arusha, Mbeya, Mwanza, Iringa,

# Wakulima, wafugaji watakiwa kuacha mazoea

Na Cheji Bakari, Kilindi

WAKULIMA na wafugaji wametakiwa kuacha maisha ya mazoea na kutambua mabadiliko yanayotokana na sheria ya matumizi bora ya ardhi na kuyapokea yanapotokea kwenye maeneo yao kuepuka migogoro isiyo lazima.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa kikao cha Amani ya wakulima na wafugaji wa Kata za Songe na Mvungwe wilayani Kilindi, Oscar Kiondo kilichofanyika hapa na kumshirikisha Katibu wa serikali ya kijiji cha Mvungwe.

Kiondo ambaye pia ni Mtendaji wa Kata ya Songe alitumia nafasi hiyo kuyaeleza makundi hayo sheria hiyo ya matumizi bora ya ardhi na wanavyotakiwa kuiishi kuondoa usumbufu.

Alieleza wajibu wa wakulima na wafugaji kutambua uwepo wa sheria ya matumizi bora ya ardhi na kujiandaa na mabadiliko yanapotokea kwenye maeneo yao badala ya kung'ang'ania maisha ya mazoea ambayo hatima ni migogoro.

Kwa upande wa maazimio ya kikao hicho, Kiondo aliagiza utekelezaji wa mambo matatu ili kukomesha migogoro hiyo, ikiwemo kupiga marufuku mfugaji kulisha mifugo kwenye shamba bila ya kupata ridhaa ya mhusika.

Mengine ni jamii kukubali mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanayotokea kulingana na wakati na kutaka jamii kutii sheria bila shuruti.

Wakizungumzia migogoro inayofukuta kati ya wakulima na wafugaji, wawakilishi wa makundi hayo kwenye kikao hicho walieleza kuwa licha ya kufanyika vikao zaidi ya vitatu, bado hakuna hatua zilizochukuliwa zaidi ya walalamikiwa.





NA LILIAN JOEL, AR

# Ng'ombe 550 waliokamatwa warejeshwa kwa wafugaji

**SERIKALI imemesema imeamua kuwarejesha ng'ombe 550 kwa wafugaji wa Kijiji cha Kimotorok, wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, bila kuwapiga faini.**

Ng'ombe hao walikamatwa na askari wa Pori la Akiba la Mkungunero kwa kosa la kuingia kwenye pori hilo kinyume cha sheria.

Akikabidhi ng'ombe hao kwa wananchi wa kijiji hicho, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel, aliwataka wafugaji kutii sheria za nchi.

"Serikali haitaki kuwaonea wananchi, hasa wafugaji, ndiyo sababu tumerejesha kwenu mifugo hii 550, iliyokuwa imeingia kwenye pori la akiba la Mkungunero. Niwaombe mtii sheria za nchi ili kuepuka usumbufu wa mifugo yenu kutaifishwa ama kupigwa faini," alisema Ole Gabriel.

Aliongeza kuwa wakati serikali ikiendelea kutafuta namna bora ya wafugaji wanaoishi pembezoni mwa hifadhi za taifa, mapori ya akiba na mapori tengefu, ni vyema wakaendelea kuheshimu sheria zilizopo ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima.

Ole Gabriel alitumia fursa hiyo kuwataka na wafugaji wote nchini, kuheshimu sheria za nchi, hasa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uhifadhi ili kuwa na uhifadhi na ufugaji endelevu.

Akizungumza kwa niaba ya wafugaji wenzake, ambao mifugo yao ilikamatwa, Lomayani Laizer, aliishukuru serikali kwa kutambua umuhimu wa wafugaji kwa sababu hawana kipato kingine wanachotegemea zaidi ya mifugo.

"Tunaishukuru serikali kwa kuturejeshea mifugo yetu kwa sababu ingetaifishwa na kupigwa mnada, tusingeruhusiwa kuinunua na ingeuzwa kwa wafugaji wengine na wafanyabiashara," alisema.

# Walimu w
# kupigwa m

**MKUU wa Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Chelestino Mofuga, ametoa onyo kali kwa wananchi wanaoishi kwenye Bonde la Yaeda Chini, kuacha kujichukulia sheria mkononi kwa kuwajeruhi walimu wanaowazuia kuchunga mifugo kwenye maeneo yasiyotakiwa.**

Tayari watu saba wanashikiliwa na polisi kwa kosa la kujichukulia sheria mkononi, ikiwa ni pamoja na kuwajeruhi walimu katika vijiji vya Endagulda na Domanga.

Akizungumza na wananchi wa vijiji hivyo mwishoni mwa wiki iliyopita, kwenye mkutano wa hadhara wa kutatua mgogoro wa walimu na wananchi, Mofuga alisema kuanzia sasa, mwananchi yeyote atakayegombana au kumjeruhi mwalimu, atachukulia hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia hiyo.

Alisema kitendo cha wananchi kuwakimbiza walimu wa shule ya msingi wakitumia mishale na kuwafanya wakimbie kituo chao cha kazi, hakiwezi kuvumiliwa kwa sababu serikali inatumia gharama

kubwa kupeleka walimu maeneo ya



**MKUU** wa w
wa Shrika la Wa
Maendeleo ya N

# 'Andikeni miradi ya m

# ...kutumia sh. ...adi ya jamii

...u katika maeneo ...mkoa wa Tanga, ...adiriwa kuwa na ...milioni 50.

...kwa kuanzia, ...a msaada katika ...i kuwahamasisha ...zaidi kusoma na ...ono serikali katika ...ure.

...katika hafla ...Wilaya ya Tanga, ...wa, aliishukuru ...huo, unaolenga ...zingira kwenye

...nsaada huo ...wanafunzi ...mazingira rafiki, ...kupata elimu ...a na kipindi hiki ...wa sayansi na

"Kiukweli tuna maelekezo ya utekelezaji kutoka kwenye bodi yetu kwa ajili ya sera ya kuchangia usaidizi miradi ya maendeleo. Hii inahusu maeneo yanayopitiwa na bandari, ...



# Wafungaji watengenezewa mazingira kupata mikopo

**SERIKALI imeendelea kutengeneza mazingira mazuri na kuiwekea mikakati sekta ya mifugo kwa lengo la kuwawezesha wafugaji kukopesheka kwenye taasisi mbalimbali za fedha hapa nchini.**

Meneja wa Kiwanda cha Maziwa cha Tanga Fresh cha Jijini Tanga, Maico Karata, alitoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita, akisema licha ya serikali kukabiliwa na changamoto nyingi kwenye sekta ya mifugo, tayari mikakati imewekwa ili kuweza kufanya maboresho.

Alisema wafugaji hawana haja ya kukata tamaa, badala yake wanatakiwa kujidhatiti kwenye shughuli hiyo, akiwasihi kufuga kisasa.

Aidha, Karata alisema serikali imejipanga kutafuta fedha kwenye benki zenye riba nafuu ili kuwakopesha wafugaji waweze kunufaika na sekta hiyo.

Alisema mipango yote hiyo inafanywa na serikali kupitia wizara ya mifugo, hivyo alitumia fursa hiyo kuwasisitiza waendelea kujikita kwenye ufugaji wa kisasa.

Mtandao hu...

**There are plenty of opportunities in the fisheries sector such as establishment of fish processing plants and modern fishing boat building yards, establishment of dry docks and eco-tourism facilities**



tegic pharmaceutical industries.

Mwambe noted that local and foreign investors may venture into agro-processing industries to add value to crops as well as livestock, forestry and fisheries products.

Other investment opportunities in the manufacturing sub-sector are sugarcane farming and establishment of processing industries, edible oil processing, gas and chemical industries particularly the construction of a liquefied natural gas (LNG) plant expected to be located in Lindi region.

In the tourism sector opportunities are available in the construction of tourist accommodation facilities, leisure parks, conference tourism facilities and provision of air/ground transport.

In ICT investors can deal with provision of mobile phone services especially in rural areas as currently penetration is higher in urban areas.

There is also the need for provision and operation of value added network for data services (internet, voice mail, electronic mail services), plus repairing and maintenance of telecommunications facilities.

He said there are infrastructure projects which provide exciting public private partnership (PPP) opportunities for investors looking to capitalize in the country's growing economy.

On precious stones and metals, opportunities are available in value addition and beneficiation of minerals such as processing of gemstones, establishment of a soda refinery plant and production of iron ore and steel in Engaruka in Arusha.

There is also need for facilities for processing of nickel in Kabanga and uranium extraction at Mkuju River in Namtumbo, Ruvuma region, he added.

# a bullion market

are more than six million small scale miners across the country.

The report also reveals that an estimated 40.5 million people were in direct engagement with artisanal and small-scale mining in 2017, up from 30 million in 2014, 13 million in 1999 and six million six years earlier.

Just last month, President John Magufuli held talks with mining sector stakeholders, with the major agenda being to devise solutions to alleviate their grievances. The meeting was also organised for the president to receive advice about the ideal strategy to employ to operate the mining sector for the benefit of Tanzania and its people. The outcomes of the forum led the United Republic to endorse a bill that removed the payment of 5 percent withholding tax and 18 percent value added tax which small-scale miners were previously mandated to pay.

There are five districts in Geita Region, namely Mbogwe, Kahama Rural, Kahama Urban, Bukombe, Chato and Geita. Each of these districts will have a centre for gold collection from small-scale miners alongside two banks where gold traded will be held for safe and secure transaction conducts.